



Kiasi Kinachotozwa kwa Kawaida

Ukipokea usaidizi chini ya Sera ya Usaidizi wa Kifedha wa CoxHealth (FAP), hospitali na kliniki* hazifai kukutoza zaidi ya kiasi cha kawaida (AGB) kinachotozwa watu wenye bima wanaopokea huduma sawa. Mgonjwa anayestahiki kupokea Usaidizi wa Kifedha anaweza tu “kutozwa” kiasi ambacho yeye mwenyewe anafaa kulipa, baada ya mapunguzo yote (yakiwemo mapunguzo yanayopatikana chini ya FAP) na malipo ya bima kutekelezwa.

CoxHealth hupata AGB kwa kuzidisha matozo ya juma la hospitali kwa huduma husika na mojawapo au mseto wa asilimia za jumla ya matozo yanayoitwa “asilimia za AGB.” Asilimia ya AGB huhesabiwa kila mwaka kwa kugawanya kiasi kamili cha madai yote ya hospitali (bila kujumuisha madai ya bima na Medicaid) ambayo yameruhusiwa na watoa bima za afya katika kipindi cha miezi 12 ya awali na jumlisho la jumla ya matozo ya madai hayo. Kwa madhumuni hayo, kiasi kamili kinachoruhusiwa mtoa bima kinacjumuisha kiasi kilichorejeshwa na mtoa huduma za bima na kiasi chchochote (ikiwa kipo) ambacho ni jukumu la mtu binafsi kulipa zikiwemo ada ya kuchangia, mchango wa bima au makato. Hesabu za

AGB hufanywa kila mwaka kwa ajili ya kila hospitali na kliniki.

Mara baada ya usatahili wa hospitali kushiriki katika Usaidizi wa Kifedha, hospitali itatumia punguzo linalofaa la Usaidizi wa Kifedha uliotajwa katika Jedwali la Mapati na Mapunguzo ya Usaidizi wa Kifedha. Kila kiasi unachotakiwa kutozwa kitakaguliwa ili kuhakikisha kwamba hakizidi asilimia ya AGB. Ikiwa kiasi unachodaiwa kinazidi kiasi kinachoruhusiwa na AGB, punguzo la ziada litawekwa kwenye salio ili kukipunguza kilingane na asilimia ya AGB.

Angalia hapa chini kuona asilimia ya AGB kwa ajili ya kila hospitali na kliniki ya CoxHealth. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu hesabu za AGB, tafadhali piga simu:

Kaunti ya Barton: 417-681-5100

Branson: 417-348-8930

Monett: 417-354-1118

Springfield: 417-269-0523

Kliniki: 417-269-4353 au 417-875-3187

Mtoa huduma	Asilimia ya Kiasi Kinachotozwa kwa Kawaida (AGB)
Hospitali ya Kaunti ya Barton	34.00%
Hospitali ya Branson	24.67%
Monett Hospital	34.08%
Springfield Hospitals	28.34%
Kliniki	53.00%

*Angalia **Kiambatisho cha 3** kwa orodha ya Kliniki

Kuanzia 11/2018